




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na: 9. Msimu wa Kilimo 2019/20

Tathmini Disemba 21-31, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Januari 01-10, 2020

Muhtasari


- Mvua zinazotarajiwa katika kipindi cha Januari 01-10, 2020 zitapelekea hali nzuri ya unyevunyevu katika udongo kwa ajili ya kilimo na malisho katika maeneo mengi ya nchi.
- Kiwango kikubwa cha hali ya unyevunyevu kinaweza kuathiri hali ya ukuaji wa mazao katika maeneo ya mabondeni.
- Wakulima, Wavuvi na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kutumia taarifa za hali ya hewa.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii ilipelekea kuendelea kusukumwa kwa ukanda wa mvua (ITCZ) kuelekea kusini hadi kufika katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani lilishuhudiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hali hiyo iliyosababisha kuimarika zaidi kwa mifumo ya mvua. Kwa upande mwingine, joto la bahari la wastani lilishuhudiwa eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilipelekea kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka magharibi ilipo misitu ya Congo.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2019

Kwa ujumla katika kipindi hiki, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua za kutosha kama inavyoonekana katika kielelezo 1. Katika baadhi ya maeneo ya ukanda unaopata mvua kwa msimu mmoja (kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, na ukanda wa kusini mwa nchi) yalipata kiasi cha mvua kuanzia 100 mm hadi 250 mm. Pia, maeneo machache ya Dodoma, Singida, Njombe, Morogoro kusini, Lindi, na Mtwara yalirekodi kiwango cha juu cha mvua kati ya 200 mm na 250 mm. Vile vile maeneo mengi ya ukanda unaopata mvua mara mbili kwa mwaka yalipata kiwango cha mvua kidogo kulinganisha na maeneo mengine kutokana na msimu wa vuli kuelekea mwishoni. Maeneo maeneo mengi yalipata kiasi cha mvua chini ya 100 mm.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Disemba 21- 31, 2019.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2019

Kiwango cha mvua kilichorekodiwa katika kipindi hiki, kilipelekea hali nzuri ya ukuaji wa mazao. Maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Kilimanjaro, Arusha, Moshi na Manyara) wakulima waliendelea na shughuli za palizi lakini kwa maeneo ya pwani ya kaskazini (Tanga, Pwani, Morogoro kaskazini, visiwani Pemba na Unguja) wakulima walianza shughuli za uvunaji wa mahindi na maharagwe. Baadhi ya maeneo katika ukanda huo iliripotiwa mahindi yapo katika hatua ya kubeba na kukomaa wakati maharagwe yapo katika hatua ya maua na kukomaa kasoro eneo la Karagwe ambapo wameanza uvunaji wa maharagwe. Ukanda wa mvua moja kwa mwaka wakulima waliendelea na upandaji wa mtama, alizeti, na mahindi hususan ukanda wa kati, pwani ya kusini, na kusini mwa nchi. Wakulima walikuwa wanafanya palizi ya mahindi na maharagwe katika eneo la magharibi mwa nchi

(Kigoma and Tabora) na viazi ulaya katika eneo la nyanda za juu kusini magharibi (Njombe and Mbeya). Zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya jani la tisa katika mikoa ya Njombe, Mbeya, Tabora, and Kigoma vilevile viazi vitamu vilikuwa katika hatua ya kuchipua kwa mikoa ya Mbeya and Njombe. Wakati mkoani Rukwa mahindi yalikuwa katika hatua ya kutoa mbelewele na maharagwe katika hatua ya kutoa maua.

Kwa ujumla katika hiki kipindi, maeneo mengi ya nchi mazao yalikuwa katika hali nzuri na ardhi ilikuwa na kiwango cha unyevu nyevu wa kutosha. Kuzidi kwa kiwango cha unyevunyevu katika baadhi ya maeneo kuliathiri ukuaji wa mazao. Kwa mfano, ugonjwa wa ukungu uliathiri viazi mviringo mkoani Njombe na mahindi kuwa njano katika baadhi ya maeneo mkoani Simiyu.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2019

Kutokana na mvua za msimu kuendelea maeneo mengi ya nchi, imepelekea kiwango cha maji katika mabwawa na mtiririko ya maji katika mito kuendelea kuongezeka.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 01-10, 2020

Kwenye kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kubaki kusini katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi, hali inayotarajiwa kusababisha kutokea kwa vimbunga. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kupelekea upepo hafifu kuvuma kutoka magharibi hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuimarisha mifumo ya unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuja katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 01-10, 2020

Katika kipindi cha dikadi hii (01–10), ukanda wa ziwa Viktoria (Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu and Mara)

pamoja na magharibi mwa nchi (Kigoma, Katavi and Tabora) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache. Upande wa nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) pamoja na Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajia kupata Mvua nyepesi katika maeneo machache. Pia, kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida), pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi), na kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajia mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo pamoja na vipindi vifupi vya upepo mkali. Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) zinatrajia mvua zinazoambatana na ngurumo na vipindi vifupi vya upepo mkali katika baadhi ya maeneo.

HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 01-10, 2020

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi zitaimarishahali ya unyevunyevu kwenye ardhi kwa ajiri ya mazao na malisho. Hata hivyo kiwango cha juu cha unyevunyevu chawezakuathiri baadhi ya mazao kama vile maharage, mahindi, na viazi mviringo katika ukanda wa chini (Mabondeni). Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuwaona mabwana shamba kwa ajili ya kupata ushauri zaidi na pia kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwenye tovuti <http://www.meteo.go.tz/> na vyombo vingine vya habari.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 01-10, 2020

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kitapungua kwa wastani, hususan katika maeneo yanayopata mvua kwa misimu miwili. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,

S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz; (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz; -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania